RASILIMALI

# Wasomi: Taifa lisitegemee gesi

**Washauri sekta mbadala ianze kutafutwa, waonya yanayotokea Venezuela**

Kelvin Matandiko, Mwananchi
kmatandiko@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Taasisi ya Utafiti wa Kupunguza Umaskini (Repoa), imetoa tahadhari kwa Serikali na Watanzania kupunguza matumaini kwenye manufaa ya gesi asilia huku ikipendekeza kuanzishwa kwa sekta endelevu itakayokuwa mbadala wa rasilimali hiyo.

Mkurugenzi wa Mipango na Utafiti wa Repoa, Dk Abel Kinyondo alisema matumaini yaliyopo ni makubwa ikilinganishwa na uhalisia kwani makosa yaliyofanyika ni kutoa nafasi kubwa kwa Watanzania kushiriki katika rasilimali hiyo wakati hawana uwezo wa kutosheleza mahitaji na ubora unaohitajika.

Kabla ya kanuni kukamilika, Sera ya Ushirikishaji na Uwezeshaji Wazawa Tanzania (LCP) ya mwaka 2014, Sera ya Gesi Asilia ya 2013 na Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Gesi Asilia ya 2015, Serikali iliweka mkakati wa kuhakikisha wazalishaji na kampuni za ndani zinanufaika kwa asilimia 25 wakati wa uzalishaji.

Akizungumza wiki iliyopita katika mafunzo ya uchambuzi wa masuala ya uchumi na mikataba ya gesi na mafuta kwa wanahabari, Dk Kinyondo alisema kinachoweza kusaidia ni Serikali kuongeza kodi na kupunguza ushiriki wa LCP kwa Watanzania ili kuepuka wajanja wachache watakaojinufaisha wakati wa uzalishaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Repoa, Dk Donald Mmari alisema endapo Taifa litakuwa na fikra ya uchumi kujengwa kwa gesi pekee ni kosa kubwa kwa kuwa baadhi ya nchi zikiwamo Angola na Venezuela zinajuta kwa sasa licha ya kupata utajiri wa rasilimali hiyo.

"Sasa tunatumiaje sekta ya gesi kuimarisha kilimo na ku-promote viwanda bila mtazamo mpana ili tusipate shida ya utegemezi. Tunaweza kujikuta kwenye matatizo yaliyojitokeza Venezuela na Angola," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Dk Godfrey Simbeye alikiri kuwapo kwa hofu ya wajanja wachache kunufaika na wazalishaji wadogo kutonufaika.

"Ni kweli wajanja wachache wenye uwezo wanaweza *ku-take advantages* (kutumia mwanya huo), lakini changamoto hiyo ni vyema ikajibiwa kwenye kanuni zitakazoandaliwa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hiyo, sijui kwa sasa imefikia wapi maandalizi yake," alisema.

> **"Venezuela sasa hivi wanapanga foleni ya mkate na utajiri wao, walijisahau kubadilisha rasilimali hiyo itumikeje kwa uchumi. Kwa mfano kilimo kinaajiri wengi ila uzalishaji hafifu."**
> Donald Mmari

MAWASILIANO

Mfanyakazi wa Kampuni ya SimbaNet, Shashi Samwel akieleza jinsi walivyobuni mnara wa mawasiliano kwenye sherehe ya Siku ya Familia iliyoandaliwa na kampuni hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki iliyopita. **Picha na Anthony Siame**



# Serikali yatangaza neema zao la chai

Florence Focus, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Tarime.** Ukiwa ni mkakati maalumu wa kufufua na kuimarisha kilimo cha chai, Serikali imepanga kupeleka miche ya ruzuku wilayani Tatime, Mkoa wa Mara ili kuongeza uzalishaji.

Mpango huo ulitangazwa juzi na Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, William ole Nasha katika ziara yake ya kuangalia na kutafutia ufumbuzi changamoto zinazozikabili sekta wanazosimamia.

Ole Nasha aliwaagiza wataalamu wa kilimo wilayani hapa kuongeza kasi ya kuwaelimisha wakulima mbinu za kilimo bora cha chai. "Kwa upande wa wizara tutahakikisha miche ya ruzuku inawafikia wakulima kwa wakati ili siyo tu waongeze uzalishaji, bali kukuza kipato chao," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Glorious Luoga alisema wakulima wengi hawajachangamkia kilimo cha zao hilo, hivyo kukifanya kiwanda cha kusindika chai kukosa malighafi ya kutosha.

Kiwanda cha Chai Tarime kina uwezo wa kuzalisha tani nane kwa siku, lakini kwa sasa kinazalisha tani moja.

Akizungumzia mazao ya chakula, Luoga alisema sehemu hiyo huzalisha zaidi ya tani 140 kila mwaka ikiwa ni ziada ya tani 89 za mahitaji ambayo ni tani 51 kwa mwaka.

"Lakini tunakabiliwa na changamoto ya wananchi kutokuwa na utamaduni wa kuhifadhi chakula cha ziada kwa mahitaji ya familia baada ya mavuno na baadhi hutumia nafaka kutengeneza pombe za kienyeji huku wengine wakiuza," alisema.


## VACANCIES

1. RADIO PROGRAM PRODUCERS – 2 POSTS
2. EDITORS....... 2 POSTS
3. ANNOUNCERS 4 POSTS;
4. Marketing officer ; ONE POST –A person with Media knowledge and experience and International marketing for Radio Broadcasting;
5. RADIO TRANSMITION TECHNICIAN – 1 post;
6. Comedians 4 posts ;
7. **EDUCATION AND QUALIFICATIONS;..........**
All must be Diploma and above from reputable institution with Knowledge and experience of not less than 3 years in the related field with knowledge of using broadcasting programmes , age between 25 to 45 years;

**EXPERIENCE;** Not less than three years in Radio Broadcast activities and working experience not less than 3 years.
Editors, Producers and announcers must be Acquainted with Radio broadcast program such as Jazla, Sum Broadcaster, Radio five and others etc;

**Send you Cv and application to Radio Kili Fm Stereo Limited , P.O.Box. 6841- Moshi or through our E- Mail kilifmradio@yahoo.com Deadline 15.12.2016**


IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(COMMERCIAL DIVISION)
AT DAR ES SALAAM
COMMERCIAL CASE NO 89 OF 20 16

BRIDGEWAYS LOGISTICS LTD .......... PLAINTIFF

VERSUS

TRIPLE 'A' HAULIERS LTD .......... DEFENDANT

SUMMONS TO APPEAR AND ANSWER THE CLAIM
(U/O V RULE 1(a) of the CPC) Cap 33 RE 2002)

To:
Petro Truck (T) Ltd
Dar Es Salaam

TAKE NOTICE that the Plaintiff has instituted a suit against you with particulars of claim set out in a plaint Annexed herewith.

You are hereby summoned to appear in this Court in person or by an Advocate or an agent duly authorised on 25th day of November 2016 At 9:00 a.m when this suit will be coming on for orders.

TAKE FURTHER NOTICE that should you default to enter appearance in Court on the day of time mentioned above, the suit will proceed and Judgment may be given in your absence.

Given under my hand and the Seal of the Court, this 15th day of Nov 2016

DEPUTY REGISTRAR

IN THE DISTRICT QCOURT FOR ILALA
AT SAMORA AVENUE
CIVIL CASE NO. 163 OF 2016

FATUMA MWAIMU
(Suing as an Attorney of MARK & ASSOCIATES ATTORNEYS __________ PLAINTIFF

VERSUS

DEVERGY EAST AFRICA LIMITED __________ DEFENDANT

SUMMONS TO APPEAR

TO
DEVERGY EAST AFRICA LIMITED

WHEREAS the above mentioned Plaintiff has instituted a suit against you at Ilala District Court the facts of which may be found on request in the Court file. Take Notice that, the case has been fixed for Mention on 23rd November, 2016 at 11:00 am before Hon. Luhwago, RM.

AND FURTHER TAKE NOTICE THAT, if you default in filling of the Written Statement of Defence within the time fixed the Court shall pronounce judgment against you.

Given under my HAND and SEAL of the Court this 15th day of November, 2016

RESIDENT MAGISTRATE
ILALA - DAR ES SALAAM
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA WILAYA ILALA